**HOTUBA YA MHESHIMIWA WILLIAM TATE OLE NASHA (MB), WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI WAKATI WA UFUNGUZI WA MKUTANO WA MADALDO NA MALDO WA KUHAMASISHA UENDELEZAJI WA TASNIA YA NYAMA NCHINI, TAREHE 26/01/2017, UKUMBI WA CHUO CHA MIPANGO-DODOMA.**

---

**Ndugu Katibu Mkuu (Mifugo) Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi**
**Ndugu Mkurugenzi waIdara ya Uzalishaji Mifugo na Masoko,**
**Ndugu Mkurugenzi Idara ya Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani**
**Ndugu Msajili wa Bodi ya Nyama,**
**Ndugu Washauri wa Mifugo**
**Ndugu Wakuu wa Idara ya Mifugo kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa,**
**Wageni Waalikwa,**
**Mabibi na Mabwana.**

**Ndugu Washiriki**, Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru waandaaji kwa kunipa fursa ya kufungua mkutano huu wa watendaji wa sekta ya Mifugo katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa. Aidha, najisikia kuwiwa kuwapongeza Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizofanikisha kuleta wajumbe kushiriki katika mkutano huu muhimu unaolenga kujadili namna bora ya kuendeleza tasnia ya nyama nchini. Hii inadhihirisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinaelewa kuwa jukumu la kuendeleza tasnia ya nyama hapa nchini ni la wadau wote. Hivyo, ninatoa wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo hazikuwakilishwa kwenye mkutano huu, kuhakikisha zinapata taarifa na kutekeleza yatakayokubaliwa katika mkutano huu. Mwisho kwa kutaja na sio kwa umuhimu, napenda kushukuru viongozi wa mkoa wa Dodoma kwa kukubali kuwa wenyeji na kwa mapokezi mazuri.

**Ndugu Washiriki,** nimeambiwa mtakuwepo hapa kwa siku moja, naamini mtaitumia vizuri siku hii kadri itakavyowezekana kujadili namna bora ya kuiendeleza tasnia ya nyama na sekta ya mifugo kwa ujumla ili kuiwezesha Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazonufaika na rasilimali zake za mifugo. Ninafahamu kwamba miongoni mwa majukumu yenu ni kusimamia utekelezaji wa Sheria zinazoongoza sekta hii kwa ujumla ikiwa ni pamoja na Sheria ya:-

- Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya Mwaka 2003;
- Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006;
- Biashara ya Ngozi na Mazao yake Na 18 ya Mwaka 2008;
- Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya Mwaka 2008;
- Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo na Mazao yake Na.12 ya Mwaka 2010; na
- Maeneo ya Malisho na Vyakula vya Mifugo Na. 13 ya Mwaka 2010.

**Ndugu Washiriki,** Aidha, utendaji kazi wenu uzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Malengo ya Kimataifa ya Millenia (MDGs) na Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). Pia kuzingatia Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006, Mkakati wa kutekeleza sera hiyo, Mpango II wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021), mpango wa kuendeleza sekta ya Kilimo – ASDP II, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2015 – 2020, Mkakati wa Taifa wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini II, Hotuba ya Rais aliyoitoa wakati wa kufungua Bunge la kumi na moja la Tanzania tarehe 20 Novemba 2015 na Mpango wa maboresho wa Serikali za Mitaa (LGRP) unaohimiza ugatuzi wa madaraka (D by D).

**Ndugu Washiriki,** napenda sasa tuangalie uwezo wa Tanzania katika kuzalisha mifugo na biashara ya nyama. Ninajivunia kwamba Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali kubwa ya eneo la malisho na mifugo. Takwimu zinaonyesha kwamba Tanzania ina ukubwa wa hekta milioni **88.6** za ardhi na kati ya hizo, hekta milioni **60** zinafaa kwa malisho ya mifugo. Tanzania kwa sasa ina idadi kubwa ya mifugo ambayo ni takribani Ng'ombe milioni **22.8,** Mbuzi milioni **15.6,** Kondoo milioni **7.0,** Nguruwe milioni **2.01**, Kuku wa asili milioni **35** na wa kisasa milioni **35.5.** Sehemu kubwa ya mifugo hii ni ya asili na inaongezeka kwa kiasi cha asilimia **3.8** kwa mwaka na kuchangia kiasi cha asilimia **4.4** katika pato la Taifa. Kama hiyo haitoshi takwimu za ulaji wa nyama nchini zinaonyesha kwamba watanzania wanakula kiasi kidogo cha nyama ambacho ni kilo **12** za nyama kwa mtu kwa mwaka ikilinganishwa na kiwango cha kilo **50** za nyama kwa mtu kwa mwaka kilichokadiriwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO).

**Ndugu Washiriki,** kutokana na takwimu hizi, ni dhahiri kwamba Tanzania ina fursa kubwa ya kuendeleza zao la nyama kibiashara na kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Takwimu za biashara ya mifugo na nyama katika mwaka 2015/2016 zinaonyesha kwamba ng'ombe **1,470,805**, mbuzi **1,161,840** na kondoo **253,243** waliuzwa. Aidha, wastani wa **tani 648,810** za nyama (tani **323,775** nyama ya ng'ombe, tani **129,292** nyama ya mbuzi na kondoo, tani **91,451** ya nguruwe na tani **104,292** nyama ya kuku) zilizalishwa ambapo asilimia **99** ya nyama hii iliuzwa katika soko la ndani.

Aidha, soko la nyama la ndani na nje ya nchi limendelea kukua, kwa mujibu wa takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba uwezo wa kuuza nyama na bidhaa zake nje ya nchi umeongezeka kutoka tani **25** kwa wiki (2014/2015) hadi tani 50 kwa wiki (2015/2016). Pamoja na ongezeko hilo, bado nchi yetu haijaweza kukidhi mahitaji ya nyama katika masoko ya nje Afrika (Misri tani 500 kwa wiki) na nchi za Falme za Kiarabu (UAE, tani 150 kwa wiki). Hata hivyo, taarifa zinaonesha kuwa katika mwaka 2015/2016, jumla ya tani **2,356.62** za nyama (tani **203.73** za nyama ya ng'ombe, tani **1,216.24** za nyama ya mbuzi, tani **324.65** za

nyama ya kondoo na tani **612** za punda) zilizouzwa katika nchi za Kuwait, Oman, Iraq, Vietnam na Malawi.

**Ndugu Washiriki,** tutakubaliana kwamba ongezeko hili la biashara ya mifugo na nyama halioani na rasilimali ya mifugo tuliyonayo hapa nchini. Hii inatokana na uvunaji mdogo wa mifugo ambao unakadiriwa kuwa pungufu ya asilimia **10** (ng'ombe) kwa mwaka, kiwango ambacho ni chini ya kiwango kinachoshauriwa cha asilimia **15** – **30** kwa mwaka. Hata hivyo, ng'ombe hao huvunwa wakiwa na umri mkubwa (kuanzia miaka 5) na kuzalisha nyama yenye ubora hafifu ukilinganishwa na ubora unaohitajika katika soko maalum. Nafahamu kwamba upo uwezekano wa kuiongezea thamani mifugo kwa kuinenepesha na kuihifadhi nyama kwenye baridi kwa muda unaoshauriwa. Hata hivyo, viwango vya uzalishaji nyama katika machinjio zilizo nyingi na maduka ya kuuzia nyama hapa nchini ni duni. Hii imesababisha kupoteza soko maalum la ndani na kulazimu kuagiza nyama kutoka nje ya nchi ambapo katika mwaka 2015/2016, jumla ya tani **1,492.20** za nyama (tani **836.13** ya ng'ombe, tani **619.46** ya nguruwe, tani **1.0** ya mbuzi na tani **35.61** ya kondoo) ziliingizwa nchini. Kinachosikitisha zaidi ni ukweli kwamba sehemu kubwa ya nyama hii inatokana na mifugo inayozalishwa hapa nchini na kuvushwa nje ya nchi kwa njia zisizo halali, kusindikwa na kurudishwa nchini.

**Ndugu Washiriki,** Sote tunafahamu kwamba sekta ya mifugo inakabiliwa na changamoto nyingi zinazokwamisha juhudi za kuongeza uzalishaji wa mifugo na nyama bora zinazokidhi mahitaji ya soko la ndani na nje. Baadhi ya changamoto hizo ni upatikanaji wa ardhi ya ufugaji na miundombinu yake, migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, ambayo wakati mwingine husababisha vifo vya watu na mifugo, upatikanaji wa mbegu bora za mifugo, kuwa na teknolijia za uzalishaji, udhibiti wa magonjwa, ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake, kuwa na muundo imara wa utawala unaowezesha biashara ya mifugo (vyama vya wadau imara), uwezo mdogo wa kimitaji, teknolojia duni, uvunaji mdogo wa mifugo na kwa wakati, uzalishaji mdogo wa nyama inayokidhi viwango vya ubora kulingana na mahitaji ya soko, kutokuwepo kwa mifumo bora ya uzalishaji wa mifugo unaohusisha hifadhi ya malisho bora, uhaba wa viwanda/machinjio za kisasa kwa ajili ya kuchinja, kuchakata na kusindika nyama, utumiaji mdogo wa uwezo wa machinjio za kisasa zilizopo.

Ni dhahiri kwamba uwekezaji katika kutatua changamoto zinazokabili sekta ya mifugo kutaleta mabadiliko makubwa na ya haraka. Kwa kuwa bado kuna fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji, hasa pale ambapo mbinu za kibiashara zitatumika kuzalisha mifugo bora kwa kulenga mahitaji ya soko na kuhamasisha uvunaji wa mifugo kwa wakati. Hivyo, ninahimiza wadau wote wanaohusika na maendeleo ya sekta ya mifugo kujikita katika kutatua changamoto zilizopo ili kuongeza kipato cha wafugaji na cha Taifa kwa ujumla.

**Ndugu Washiriki,** nimeambiwa kwamba mkutano huu ni kiutendaji na umejumuisha watendaji wa sekretariati za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ninaamini kwamba mtajadiliana kwa kina na kukubaliana namna ya kutekeleza majukumu yenu kwa ufanisi na kuleta tija kwenye tasnia ya nyama na sekta ya mifugo kwa ujumla. Hivyo, ninasisitiza katika majadiliano yenu mjikite kujadili namna ambavyo mtatekelezaji wa mambo yafuatayo pamoja na majukumu yenu ya msingi;

- Kuzielewa vizuri sheria zinazosimamia maendeleo ya sekta ya mifugo ili kusimamia utekelezaji wake kwa ufanisi;
- Kujihusisha kwa karibu katika kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kupunguza au kumaliza kabisa migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na watumiaji wengine kwa kutambua, kutenga, kulinda maeneo ya ufugaji kisheria na kuyaendeleza ili kuhakikisha malisho na maji ya kutosha yanapatikana wakati wote;
- Kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu ufugaji wa kibiashara na kuvuna kwa wakati ili kupata mifugo bora inayohitajika kuzalisha nyama bora katika machinjio na viwanda vya kusindika na kuongeza thamani ya nyama;
- Kutambua na kuorodhesha wafugaji wa mifugo inayozalisha nyama (ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, sungura, nguruwe na punda) na kuwajengea uwezo wa kuboresha mifugo hiyo kwa kutumia teknolojia mbalimbali kama vile kuchagua (selection) koosafu bora za nyama zinazofaa kuzaliana na kuhasi zile zisizofaa;
- Kuhimiza uanzishaji na uendeshaji wa minada uzingatie sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa ikiwa ni pamoja na kuhimiza matumizi ya mizani na kutumia utaratibu wa kuuza mifugo kwa kunadi ili kumwezesha mfugaji kupata bei stahili ya mifugo yake;
- Kuhimiza matumizi ya mizani za kisasa (digital) katika biashara ya nyama ili kuwezesha walaji kununua nyama kulingana na kiasi cha fedha aliyonayo na hivyo kuongeza ulaji wa nyama;
- Kutekeleza majukumu yenu ya msingi katika utoaji wa huduma mbali mbali zikiwemo elimu kwa wafugaji kuhusu uzalishaji, uhifadhi na utumiaji wa malisho na vyakula vya mifugo, ushauri kwa wafugaji kuhusu utunzaji bora wa mifugo;
- Kutoa taarifa na takwimu sahihi kwa wakati kuhusu udhibiti wa magonjwa na usimamizi wa utekelezaji wa sheria;
- Kuhakikisha vyama vya wadau vinatambulika, vinaimarishwa na kuunganishwa na huduma za kifedha na masoko;

- Kuhakikisha biashara haramu ya mifugo na nyama kwenda nchi jirani kupitia katika mipakani isiyo rasmi bila kufuata taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria inadhibitiwa;
- Kuhakikisha wafugaji wanasajili mifugo yao kwa ajili ya ufuatiliaji wa mazao ya mifugo,
- Kusajili wadau wote wa tasnia ya nyama ili kazi zao zitambuliwe na mchango wao katika maendeleo ya tasnia ufahamike.

**Ndugu Washiriki,** ninasisitiza kuhusu utekelezaji wa zoezi zima la utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake kutokana na umuhimu wake katika biashara ya mifugo na mazao yake. Mfumo huu unatumika duniani kote na unahimizwa na Shirika la Kimataifa la Biashara Duniani (WTO) kupitia Shirika la Afya ya Wanyama (OIE) kama mfumo wa kusimamia usalama wa vyakula vitokanavyo na mazao ya kilimo na vyenye asili ya mifugo (SPS). Kwa kuzingatia azima ya Serikali ya kukuza uchumi wa viwanda, sekta ya mifugo pia inahamasisha uwekezaji katika viwanda vya kusindika nyama na bidhaa zake zenye ubora zitakazoweza kupenya katika masoko kwingineko duniani. Hivyo, utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo na bidhaa zake ni jambo ambalo haliepukiki na njia rahisi ni upigaji chapa. Kwa sasa Upigaji Chapa ng'ombe ni amri ambayo ni lazima itekelezwe kwa umakini mkubwa kama ilivyotolewa na Waziri Mkuu na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Ndugu Washiriki,** ni matarajio yangu kwamba mtashiriki kikamilifu katika majadiliano ili kila mshiriki aelewe jukumu lake katika kuendeleza tasnia ya nyama. Baada ya kusema haya machache, napenda sasa kutamka kuwa Mkutano huu **umefunguliwa rasmi**.

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**